

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



14 JUNI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI – TAREHE 14 JUNI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/2022 na Tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**410. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI
(MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-


Je, mpaka sasa ni Wawekezaji wangapi wamemilikishwa ardhi na kupata Hati kuitia Kituo cha Uwekezaji (TIC).

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

411. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILI ZODO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Sekta ya Afya nchini ina upungufu wa Watumishi wapatao 16,000:-

- Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na changamoto hiyo.



WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

412. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Bandari ya Uvubi na kununua Meli ya Uvubi katika Mkoa wa Mtwara.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

413. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mpango wa uvunaji wa Mikoko kwa Wananchi wanaoishi maeneo ya Delta wanaotegemea zao hilo kuendesha shughuli zao.

WIZARA YA MAJI:

414. MHESHIMIWA SILLO DANIEL BARAN (BABATI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza upembuzi yakinifu na ujenzi wa miundombinu ya maji katika Ziwa Madunga ili kutatua tatizo sugu la maji katika Kata ambazo hazina maji katika Jimbo la Babati Vijijini.

415. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ujenzi wa Mradi wa Maji katika Mji Mdogo wa Chala ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za Mwaka 2020.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

416. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya kutoka Mnivata hadi Masasi kupitia Newala utaanza.

417. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Je, ni lini Bandari ya Sota eneo la Shirati itaanza kurekebishwa ili kuinua Uchumi na kuboresha shughuli za Kibashara katika eneo la Mpakani mwa Tanzania na Kenya.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

418. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusomesha Wahadhiri wengi zaidi katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (PhD) kwani waliopo sasa ni wachache.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

419. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha zoezi la utoaji wa Vitambulisho vya Taifa kwa Wananchi kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa Vitambulisho hivyo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



DODOMA
14 JUNI, 2021

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE